



## **Yakwamba Mtume -rehema na amani ziwe juu yake- alikuwa anapo swalí anatanua kati ya mikono yake mpaka unaonekana weupe wa kwapa zake**

Kutoka kwa Abdallah bin Maliki bin Buhaina radhi za Allah ziwe juu yake: Yakwamba Mtume -rehema na amani ziwe juu yake- alikuwa anapo swalí anatanua kati ya mikono yake mpaka unaonekana weupe wa kwapa zake.

[Sahih] [Wamekubaliana Bukhaariy na Muslim]

Alikuwa rehema na amani zimshukie anaposwali, anaikunjua mikono yake wakati wa kusujudu. Alisogeza kila mkono kutoka upande wa karibu yake, kama mbawa mbili, mpaka rangi ya ngozi ya makwapa yake inaonekana; Hii ni katika kupitiliza kuitanua mikono na kuitenganisha na mbavu zake.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/3220>

النّجّات الخيريّة  
ALNAJAT CHARITY



لجنة الدعوة الإلكترونية  
E-Da'wah Committee

